**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA WIZARA YA ELIMU,**
**SAYANSI NA TEKNOLOJIA**


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI
NA TEKNOLOJIA

Cheti cha Ithibati

Na. 997

Jina la Chapisho: Muhtasari wa Somo la Jiografia na Mazingira Elimu ya Msingi Darasa la III - VI

Mchapishaji: Taasisi ya Elimu Tanzania

Mwandishi: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

ISBN: 978-9987-09-802-6

Muhtasari huu umeidhinishwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia tarehe 29 Juni 2023 kuwa Muhtasari wa Somo la Jiografia na Mazingira Elimu ya Msingi Darasa la III - VI Tanzania Bara.

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa
Kamishna wa Elimu

# MUHTASARI WA SOMO LA MBINU ZA UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI JIOGRAFIA NA MAZINGIRA

## STASHAHADA YA UALIMU ELIMU YA MSINGI

2023

Muhtasari wa mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa Jiografia na Mazingira, Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi.indd 1 19/10/2024 14:35

©Taasisi ya Elimu Tanzania 2023

Toleo la Kwanza 2023

ISBN 978-9987-09-801-9

Taasisi ya Elimu Tanzania
Eneo la Mikocheni
132 Barabara ya Ali Hassan Mwinyi
S. L. P. 35094
14112 Dar es Salaam

Simu: +255 735 041 168/ +255 735 041 170
Baruapepe: director.general@tie.go.tz
Tovuti: www.tie.go.tz

Muhtasari huu urejelewe kama: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (2023). *Muhtasari wa mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa Jiografia na Mazingira; Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi*. Taasisi ya Elimu Tanzania.

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kurudufu, kuchapisha, kutafsiri wala kutoa muhtasari huu kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi kutoka Tasisi ya Elimu Tanzania.



Muhtasari wa mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa Jiografia na Mazingira, Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi.indd 2 19/10/2024 14:35

# Yaliyomo


Orodha ya majedwali ..... iv
Vifupisho ..... v
Shukrani ..... vi

1.0 Utangulizi ..... 1
2.0 Malengo Makuu ya Elimu Tanzania ..... 1
3.0 Malengo ya Elimu ya Ualimu ..... 2
3.1 Lengo kuu la Elimu ya Ualimu ..... 2
3.2 Malengo Mahususi ya Elimu ya Ualimu ..... 2
4.0 Umahiri wa Jumla wa Mafunzo ya Stashahada ya Elimu ya Ualimu ..... 2
5.0 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi ..... 3
6.0 Majukumu ya Mkufunzi, Mwalimu Tarajali na Mzazi katika Ufundishaji na Ujifunzaji ..... 4
6.1 Mkufunzi ..... 4
6.2 Mwalimu tarajali ..... 4
6.3 Mzazi/mlezi ..... 4
7.0 Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji ..... 5
8.0 Zana za Ufundishaji na Ujifunzaji ..... 5
9.0 Upimaji wa Maendeleo ya Ujifunzaji ..... 5
10.0 Idadi ya Vipindi ..... 6
11.0 Maudhui ya Ufundishaji na Ujifunzaji ..... 6
Bibliografia ..... 17

## Orodha ya Majedwali


Jedwali Na. 1:Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi kwa Mwalimu Tarajali....3
Jedwali Na. 2: Mchanganuo wa Alama za Upimaji Endelevu....6
Jedwali Na. 3: Maudhui ya Mwaka wa I....7
Jedwali Na. 4: Maudhui ya Mwaka wa II....13

## Vifupisho

| | |
|---|---|
| TEHAMA | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |



Muhtasari wa mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa Jiografia na Mazingira, Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi.indd 5 19/10/2024 14:35

# Shukurani

Maandalizi ya Muhtasari wa somo la Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa Jiografia na Mazingira katika ngazi ya Stashahada ya Ualimu wa Elimu ya Msingi yamehusisha wataalamu mbalimbali kutoka taasisi za umma na zisizo za umma. Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) inatambua na kuthamini michango ya washiriki wote waliofanikisha uandaaji wa muhtasari huu. Aidha, TET inatoa shukurani za pekee kwa wahadhiri, wakufunzi, wathibiti ubora wa shule, walimu pamoja na wakuza mitaala wa TET. Vilevile, TET inaishukuru Kamati ya Kitaifa ya Wataalamu ya Kusimamia Kazi ya Maboresho ya Mitaala ya Elimu ya awali, Msingi, Sekondari na Ualimu iliyoteuliwa na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia. Kamati hii ilifanya kazi kwa weledi na kuhakikisha kuwa maudhui ya muhtasari huu yanalenga kuwa na wahitimu wenye maarifa, ujuzi na stadi zitakazowawezesha kujiajiri, kuajiriwa na kumudu maisha yao ya kila siku, ambalo ndio lengo kuu la uboreshaji wa Mitaala ya Mwaka 2023.

Mwisho, TET inatoa shukurani za pekee kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kuwezesha uandaaji na usambazaji wa muhtasari huu.

Dkt. Aneth A. Komba
Mkurugenzi Mkuu
**Taasisi ya Elimu Tanzania**

## 1.0 Utangulizi

Somo la Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji Jiografia na Mazingira Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi ni la lazima kwa mwalimu tarajali atakeyefundisha Somo la Jiografia na Mazingira ngazi ya Elimu ya Msingi. Pia, somo hili litamwezesha mwalimu tarajali kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Jiografia na Mazingira. Aidha, atakuza umahiri wa kuchambua na kutumia mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa ramani, utunzaji wa mazingira, mfumo wa jua, na tabianchi ndani na nje ya darasa.

Muhtasari huu umeandaliwa kwa lengo la kumuongoza mkufunzi katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji wa Jiografia na Mazingira Tanzania Bara. Aidha, muhtasari huu umetafsiri Mtaala wa Mafunzo ya Stashahada ya Ualimu Elimu ya msingi wa Mwaka 2023. Muhtasari utamwezesha mkufunzi kupanga shughuli za ufundishaji na ujifunzaji kwa kumjengea mwalimu tarajali stadi za udadisi, ubunifu, ushirikiano, mawasiliano na utatuzi wa changamoto katika mazingira yake. Vilevile, mwalimu tarajali atajifunza namna ya kuchopeka masuala mtambuka na kutumia TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji.

## 2.0 Malengo Makuu ya Elimu Tanzania

Malengo makuu ya elimu Tanzania ni kumwezesha kila Mtanzania:

(a) Kukuza na kuboresha haiba yake ili aweze kujithamini na kujiamini;
(b) Kuheshimu utamaduni, mila na desturi za Tanzania, tofauti za kitamaduni, utu, haki za binadamu, mitazamo na matendo jumuishi;
(c) Kukuza maarifa na kutumia sayansi na teknolojia, ubunifu, fikra tunduizi, uvumbuzi, ushirikiano, mawasiliano na mtazamo chanya katika maendeleo yake binafsi, na maendeleo endelevu ya taifa na dunia kwa ujumla;
(d) Kuelewa na kulinda tunu za taifa ikiwa ni pamoja na utu, uzalendo, uadilifu, umoja, uwazi, uaminifu, uwajibikaji na lugha ya taifa;
(e) Kujenga stadi za maisha na stadi za kazi ili kuongeza ufanisi katika maisha ya kila siku;
(f) Kukuza tabia ya kupenda na kuheshimu kazi ili kuongeza tija na ufanisi katika uzalishaji na utoaji wa huduma;
(g) Kutambua na kuzingatia masuala mtambuka, ambayo ni pamoja na afya na ustawi wa watu (jamii), usawa wa kijinsia, usimamizi na utunzaji endelevu wa mazingira; na
(h) Kukuza ushirikiano wa kitaifa na kimataifa, amani na haki kwa kuzingatia Katiba ya nchi na mikataba ya kimataifa.



Muhtasari wa mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa Jiografia na Mazingira, Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi.indd 1 19/10/2024 14:35

## 3.0 Malengo ya Elimu ya Ualimu

### 3.1 Lengo kuu la Elimu ya Ualimu

Lengo kuu la elimu ya ualimu ni kumwandaa mwalimu mwenye weledi na umahiri wa kuwezesha ufundishaji na ujifunzaji unaoendana na mabadiliko ya kisayansi, kiteknolojia, na kijamii ili kumjenga Mtanzania mwenye maarifa, stadi na mitazamo chanya, na anayethamini usawa, haki na elimu bila ukomo.

### 3.2 Malengo Mahususi ya Elimu ya Ualimu

Malengo ya Elimu ya Ualimu ni kumwandaa mwalimu kuwa mahiri katika:

(a) Kukuza uelewa wa kinadharia wa elimu ya ualimu, maadili ya kazi ya ualimu, maadili ya maisha, na misingi ya ualimu;
(b) Kujenga umahiri katika mbinu za kufundishia na kujifunzia;
(c) Kujenga umahiri katika mbinu za upimaji na tathmini kwa kuzingatia dhana ya ujenzi wa umahiri;
(d) Kukuza ubunifu na uvumbuzi katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia mahitaji ya mwanafunzi;
(e) Kutumia TEHAMA na teknolojia saidizi katika ufundishaji na ujifunzaji;
(f) Kukuza stadi za utambuzi wa awali kwa mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu ya ujifunzaji na kutoa afua stahiki;
(g) Kuimarisha matumizi ya lugha faafu katika ufundishaji na ujifunzaji; na
(h) Kujenga stadi zinazolenga kuboresha ujifunzaji, ufundishaji na upimaji (yaani *classroom- based research*).

## 4.0 Umahiri wa Jumla wa Mafunzo ya Stashahada ya Elimu ya Ualimu

Umahiri wa jumla umejikita katika misingi ya kuwasiliana, kushirikiana, ubunifu, fikra tunduizi na utatuzi wa matatizo, ujuzi wa kidijitali na uzalendo ambao umefafanuliwa katika maeneo ya ujifunzaji na masomo kama ifuatavyo:

(a) Kutumia nadharia na misingi ya ualimu katika ufundishaji na ujifunzaji;
(b) Kumudu mbinu za kufundishia na kujifunzia;
(c) Kumudu mbinu za upimaji na tathmini kwa kuzingatia ujenzi wa umahiri;
(d) Kumudu mbinu za ubunifu na uvumbuzi katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia mahitaji ya wanafunzi;
(e) Kutumia TEHAMA na teknolojia saidizi katika ufundishaji na ujifunzaji;
(f) Kutambua mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu ya ujifunzaji na kutoa afua stahiki;



Muhtasari wa mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa Jiografia na Mazingira, Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi.indd 2 19/10/2024 14:35

(g) Kutumia lugha husika kwa ufasaha katika ufundishaji na ujifunzaji;
(h) Kutumia stadi za uongozi katika taaluma (*instructional leadership*); na
(i) Kumudu stadi zinazolenga kuboresha ufundishaji, ujifunzaji na upimaji (yaani *classroom- based research*).

## 5.0 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi

Sehemu hii inawasilisha umahiri mkuu na umahiri mahususi unaotarajiwa kujengwa na mwalimu tarajali kama ulivyoainishwa katika Jedwali Na.1.

**Jedwali Na. 1:***Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi kwa Mwalimu Tarajali*

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi |
|---|---|
| 1.0 Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa Jiografia na Mazingira katika Elimu ya Msingi | 1.1 Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa ramani |
| | 1.2 Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa mfumo wa jua |
| | 1.3 Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa sura ya nchi, rasilimali na matumizi yake |
| | 1.4 Kumudu ufaraguzi na matumizi ya teknolojia na vifaa vingine saidizi katika ufundishaji na ujifunzaji wa Jiografia na Mazingira |
| | 1.5 Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa uhusiano kati ya mtawanyiko wa watu na matumizi ya rasilimali |
| | 1.6 Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa utunzaji wa mazingira na tabianchi |
| | 1.7 Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa Jiografia na Mazingira nje ya darasa |

## 6.0 Majukumu ya Mkufunzi, Mwalimu Tarajali na Mzazi katika Ufundishaji na Ujifunzaji

Ufundishaji na ujifunzaji unategemea ushirikiano madhubuti baina ya mwalimu tarajali, mkufunzi na mzazi/mlezi katika kutekeleza majukumu mbalimbali. Majukumu yao ni kama yafuatayo:



Muhtasari wa mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa Jiografia na Mazingira, Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi.indd 3 19/10/2024 14:35

**6.1 Mkufunzi**

Mkufunzi anatarajiwa:

(a) Kukuza ufundishaji na ujifunzaji unaozingatia ujenzi wa stadi za karne ya 21 kwa kutumia mbinu mbalimbali za uwezeshaji zitakazomfanya mwalimu tarajali kuwa kitovu cha ujifunzaji. Baadhi ya mbinu zinazopendekezwa ni zile zinazosaidia kukuza uwezo wa kufikiri, kutafakari, kutafuta maarifa kutoka vyanzo mbalimbali ili kutatua changamoto za ufundishaji na ujifunzaji;

(b) Kuandaa mazingira wezeshi ya kufundishia na kujifunzia ikiwa ni pamoja na kufaragua zana;

(c) Kutoa malezi kwa haki na usawa kwa kila mwalimu tarajali bila kujali tofauti zao; na

(d) Kubaini mahitaji maalumu ya mwalimu tarajali na kumpatia afua stahiki.

**6.2 Mwalimu tarajali**

Mwalimu tarajali anatarajiwa:

(a) Kushiriki kikamilifu katika shughuli za mafunzo ndani na nje ya darasa ili kuhakikisha kuwa anajenga umahiri stahiki katika maeneo mbalimbali ikiwemo usimamizi wa ufundishaji na ujifunzaji, mbinu za kufundishia na mbinu za upimaji zitakazomwezesha kubaini mafanikio na kuboresha ufundishaji na ujifunzaji;

(b) Kushiriki katika mafunzo endelevu kupitia shule zilizo jirani na chuo kwa lengo la kutafsiri nadharia anazojifunza darasani kwa vitendo. Baadhi ya nadharia hizo ni haiba, maandalizi ya somo, kutumia mbinu za kufundishia na kujifunzia, kuandaa na kutumia vifaa vya kufundishia na kujifunzia na kumthamini mwanafunzi;

(c) Kufanya kazi chini ya uangalizi wa walimu wazoefu kwa kipindi cha mwaka mmoja ili kuimarisha umahiri na weledi katika fani ya ualimu;

(d) Kushirikiana na wenzake pamoja na mkufunzi katika mchakato wa ujifunzaji; na

(e) Kuzingatia kanuni na taratibu za chuo.

**6.3 Mzazi/mlezi**

Mzazi/mlezi anatarajiwa:

(a) Kusimamia na kufuatilia mwenendo na maendeleo ya mwalimu tarajali katika ujifunzaji; na

(b) Kumpatia mwalimu tarajali mahitaji muhimu pamoja na vifaa vinavyotumika katika ujifunzaji.

**7.0 Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji**

Muhtasari huu unasisitiza matumizi ya mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazolenga kumwezesha mwalimu tarajali kuwa kitovu cha ujifunzaji na mkufunzi kuwa mwezeshaji. Mkufunzi atatumia mbinu shirikishi kumwezesha mwalimu tarajali kuwasiliana



Muhtasari wa mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa Jiografia na Mazingira, Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi.indd 4 19/10/2024 14:35

na kuwasilisha taarifa za kitaaluma na kitaalamu kwa kuzingatia mahitaji anuwai na uwezo wake. Mbinu hizo ni pamoja na zile zinazomwezesha mwalimu tarajali kufikiri kitunduizi, kutafuta maarifa kutoka vyanzo mbalimbali na kushiriki katika kutoa mrejesho. Njia nyingine ni majadiliano katika vikundi; maigizo dhima; kazimradi; fikiri-andika-jozisha-shirikisha; utafiti; utunzi wa hadithi; uwasilishaji; masimulizi; michezo mbalimbali na mbinu zingine kama hizo kulingana na muktadha ili kufanikisha ujifunzaji. Mkufunzi anashauriwa kumwongoza mwalimu tarajali kuwa mbunifu na mnyumbufu katika kutumia mbinu shirikishi wakati wa mazoezi ya ufundishaji na kufaragua zana za ufundishaji na ujifunzaji kwa kutumia mazingira halisi ya mwanafunzi.

## 8.0 Zana za Ufundishaji na Ujifunzaji

Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinapaswa kuwa shirikishi na zinazokidhi mahitaji ya ujifunzaji na uwezo wa mwalimu tarajali. Mkufunzi anapaswa kuhakikisha mwalimu tarajali anapata nafasi ya kuona, kunusa, kuonja, kusikia na kushika zana bila kuhatarisha afya ya mwalimu tarajali. Aidha, zana za ujifunzaji na ufundishaji zinapaswa kumsaidia mwalimu tarajali kuelewa kinachofundishwa. Mkufunzi anashauriwa kutumia zana zinazopatikana katika mazingira yanayomzunguka. Zana za ufundishaji na ujifunzaji zilizopendekezwa ni pamoja na vitu halisi, kompyuta, picha, michoro, ramani na kamusi mbalimbali za Jiografia. Aidha, mkufunzi anapaswa kuhakikisha kuwa mwalimu tarajali anapata nafasi ya kujifunza uandaaji na utumiaji wa zana mbalimbali za ufundishaji na ujifunzaji.

## 9.0 Upimaji wa Maendeleo ya Ujifunzaji

Upimaji wa maendeleo ya ujifunzaji ni mchakato muhimu katika ufundishaji na ujifunzaji. Upimaji wa somo la Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa Jiografia na mazingira utafanyika sambamba na masomo mengine yanayofundishwa katika ngazi ya Elimu ya Stashahada Elimu ya Msingi. Upimaji huu utamwezesha mkufunzi kupima umahiri wa mwalimu tarajali katika kumudu misingi ya mbinu za ufundishaji na ujifunzaji katika elimu ya msingi na kutumia matokeo ya upimaji kutathmini maendeleo ya mwalimu tarajali. Upimaji na tathmini ya maendeleo ya mwalimu tarajali uzingatie usawa wa kijinsia na ujumuisho. Upimaji wa maendeleo utazingatia vigezo vilivyoainishwa katika kila shughuli ya ujifunzaji. Kwahiyo, zana zinazotumika katika upimaji ni pamoja na mazoezi, maswali ya ana kwa ana, majaribio, hojaji, mkoba wa kazi, shajara, kazi mradi, uwasilishaji darasani na mitihani ya mwisho wa muhula.

Mkufunzi anapaswa kubuni shughuli nyingi zaidi za upimaji ili kuchochea ujifunzaji. Upimaji wa mwisho utachangia asilimia sabini (70%) na upimaji endelevu utachangia asilimia thelathini (30%). Mwalimu tarajali anapaswa kufaulu upimaji endelevu kwa



Muhtasari wa mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa Jiografia na Mazingira, Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi.indd 5 19/10/2024 14:35

angalau asilimia 50% na upimaji tamati kwa angalau kiwango hicho hicho ili aweze kutunukiwa cheti. Endapo hatafaulu, mwalimu tarajali anaweza kurudia mitihani hiyo mara mbili ndani ya miaka mitatu. Jedwali Na. 2 linaonesha mgawanyo wa alama katika upimaji endelevu.

**Jedwali Na. 2:** *Mchanganuo wa Alama za Upimaji Endelevu*

| Na | Shughuli ya Upimaji | (%) Mgawanyo wa Asilimia |
|---|---|---|
| 1 | Mtihani wa Muhula wa Kwanza wa Mwaka wa Kwanza | 6.0 |
| 2 | Mtihani wa Muhula wa Mwisho wa Mwaka wa Kwanza | 6.0 |
| 3 | Mtihani wa Muhula wa Kwanza wa Mwaka wa Pili | 6.0 |
| 4 | Kazi mradi | 7.0 |
| 5 | Mkoba wa Kazi | 5.0 |
| | **Jumla** | **30** |

## 10.0 Idadi ya Vipindi

Muhtasari wa somo la Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa Jiografia na Mazingira Elimu ya Ualimu unatoa makadirio ya muda utakaotumika katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia uzito wa umahiri mahususi na shughuli za kutendwa na mwalimu tarajali. Makadirio haya ya muda yamewekwa kwa mfumo wa vipindi ambapo kila kipindi ni saa moja (1). Idadi ya vipindi kwa somo hili ni vitano (5) kwa wiki kwa mwaka wa kwanza na wa pili.

## 11.0 Maudhui ya Ufundishaji ma Ujifunzaji

Muhtasari wa somo la Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa Jiografia na Mazingira mwaka wa kwanza na wa pili umebeba maudhui ambayo yamepangiliwa katika vipengele sita ambavyo ni umahiri mkuu, umahiri mahususi, shughuli za ujifunzaji, vigezo vya upimaji, zana zinazopendekezwa pamoja na idadi ya vipindi kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 3 na 4.



Muhtasari wa mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa Jiografia na Mazingira, Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi.indd 6 19/10/2024 14:35

**Jedwali Na. 3:** *Maudhui ya Mwaka wa I*

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| 1.0 Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa Jiografia na Mazingira katika Elimu ya Msingi | 1.1 Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa ramani | (a) Kumudu matumizi ya sanaa na michezo katika ufundishaji na ujifunzaji wa ramani | Sanaa na michezo katika ufundishaji na ujifunzaji wa ramani imetumika | Video yenye maudhui ya namna ya kufundisha ramani kwa kutumia sanaa na michezo<br>Hadithi ya kubuni ya ramani ya darasa, shule, wilaya na Tanzania<br>Mafumbo ya ramani (Map puzzels)- yenye maumbo mbalimbali ya ramani ya darasa, shule, wilaya na Tanzania | 50 |
| | | (b) Kumudu matumizi ya mbinu anuai za ufundishaji na ujifunzaji wa ramani katika darasa kubwa | Mbinu anuai za ufundishaji na ujifunzaji wa ramani katika darasa kubwa zimetumika | Atlas, ramani na video mbalimbali za ramani ya shule, kata na Tanzania | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (c) Kumudu matumizi ya mbinu za kuchopeka masuala mtambuka katika ufundishaji na ujifunzaji wa ramani | Mbinu za kuchopeka masuala mtambuka katika ufundishaji na ujifunzaji wa ramani zimetumika | Atlas, ramani zinazoonesha idadi ya watu, na mtawanyiko wa rasilimali | |
| | | (d) Kumudu matumizi ya mbinu za kuchopeka TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa ramani | Mbinu za kuchopeka TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa ramani zimetumika | Ramani za Tanzania za kwenye mtandao zinazoshirikisha mfano *Google Earth* | |
| | | (e) Kumudu matumizi ya mbinu nyinginezo za ufundishaji na ujifunzaji wa ramani | Mbinu nyinginezo za ufundishaji na ujifunzaji wa ramani zimetumika | Ramani za kubuni za shule, kata, Tanzania | |


Muhtasari wa mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa Jiografia na Mazingira, Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi.indd 8 19/10/2024 14:35

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | 1.2 Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa mfumo wa jua | (a) Kumudu matumizi ya sanaa na michezo katika ufundishaji na ujifunzaji wa mfumo wa jua | Sanaa na michezo katika ufundishaji wa mfumo wa jua imetumika | Atlasi, tufe, kurunzi, kifani na igizo dhima la mfumo wa jua | 40 |
| | | (b) Kumudu matumizi ya mbinu anuai za ufundishaji na ujifunzaji wa mfumo wa jua katika darasa kubwa | Mbinu anuai za ufundishaji na ujifunzaji wa mfumo wa jua katika darasa kubwa zimetumika | Video ya mfumo wa jua | |
| | | (c) Kumudu matumizi ya mbinu za kuchopeka TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa mfumo wa jua | Mbinu za kuchopeka TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa mfumo wa jua zimetumika | | |



Muhtasari wa mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa Jiografia na Mazingira, Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi.indd 9 19/10/2024 14:35

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (d) Kumudu matumizi ya mbinu nyinginezo za ufundishaji na ujifunzaji wa mfumo wa jua | Mbinu nyinginezo za ufundishaji na ujifunzaji wa mfumo wa jua zimetumika | Tufe, kurunzi, na kifani cha mfumo wa jua | |
| | 1.3 Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa sura ya nchi, rasilimali na matumizi yake | (a) Kumudu matumizi ya sanaa na michezo katika ufundishaji na ujifunzaji wa sura ya nchi, rasilimali na matumizi yake | Sanaa na michezo katika ufundishaji na ujifunzaji wa sura ya nchi, rasilimali na matumizi yake imetumika | Video zenye maudhui ya sura ya nchi | 40 |
| | | (b) Kumudu matumizi ya mbinu anuai za ufundishaji na ujifunzaji wa sura ya nchi, rasilimali na matumizi yake katika darasa kubwa | Mbinu anuai za kukabiliana na darasa kubwa katika ufundishaji na ujifunzaji wa sura ya nchi, rasilimali na matumizi yake zimetumika | | |



Muhtasari wa mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa Jiografia na Mazingira, Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi.indd 10 19/10/2024 14:35

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (c) Kumudu matumizi ya mbinu za kuchopeka masuala mtambuka katika ufundishaji na ujifunzaji wa sura ya nchi, rasilimali na matumizi yake | Mbinu za kuchopeka masuala mtambuka katika ufundishaji na ujifunzaji wa sura ya nchi, rasilimali na matumizi yake zimetumika | | |
| | | (d) Kumudu matumizi ya mbinu za kuchopeka TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa sura ya nchi, rasilimali na matumizi yake | Mbinu za kuchopeka TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa sura ya nchi, rasilimali na matumizi yake zimetumika | *Google Earth* na *google map* kutafuta maudhui ya sura ya nchi na rasilimali | |



Muhtasari wa mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa Jiografia na Mazingira, Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi.indd 11 19/10/2024 14:35

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (e) Kumudu matumizi ya mbinu nyinginezo za ufundishaji na ujifunzaji wa sura ya nchi, rasilimali na matumizi yake | Mbinu nyinginezo za ufundishaji na ujifunzaji wa sura ya nchi, rasilimali na matumizi yake zimetumika | Video yenye maudhui ya sura ya nchi | |
| | 1.4 Kumudu ufaraguzi na matumizi ya teknolojia na vifaa vingine saidizi katika ufundishaji na ujifunzaji wa Jiografia na Mazingira | (a) Kumudu ufaraguzi wa vifaa saidizi sahili katika ufundishaji na ujifunzaji wa Jiografia na Mazingira | Ufaraguzi wa vifaa saidizi sahili katika ufundishaji na ujifunzaji wa Jiografia na Mazingira umefanyika | Makunzi, vitu halisi, michoro, ramani na picha | 40 |
| | | (b) Kumudu matumizi ya teknolojia na vifaa vingine saidizi katika ufundishaji na ujifunzaji wa Jiografia na Mazingira | Teknolojia na vifaa vingine saidizi katika ufundishaji na ujifunzaji wa Jiografia na Mazingira vimetumika | Video, kinyonyeo (flash), vitumilaini (software) vitumivigumu (hardware), zenye maudhui ya Jiografia na Mazingira | |



Muhtasari wa mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa Jiografia na Mazingira, Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi.indd 12 19/10/2024 14:35

**Jedwali Na. 4:** *Maudhui ya Mwaka wa II*

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| 1.0 Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa Jiografia na Mazingira katika Elimu ya Msingi | 1.5 Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa uhusiano kati ya mtawanyiko wa watu na matumizi ya rasilimali | (a) Kumudu matumizi ya sanaa na michezo katika ufundishaji na ujifunzaji wa uhusiano kati ya mtawanyiko wa watu na matumizi ya rasilimali | Sanaa na michezo katika ufundishaji na ujifunzaji wa uhusiano kati ya mtawanyiko wa watu na matumizi ya rasilimali zimetumika | Ramani zinazoonesha mtawanyiko wa watu, na rasilimali, igizo lenye maudhui ya namna rasilimali zinavyotumika | 80 |
| | | (b) Kumudu matumizi ya mbinu anuai za ufundishaji na ujifunzaji wa uhusiano kati ya mtawanyiko wa watu na matumizi ya rasilimali katika darasa kubwa | Mbinu anuai za kukabiliana na darasa kubwa katika ufundishaji na ujifunzaji wa uhusiano kati ya mtawanyiko wa watu na matumizi ya rasilimali, zimetumika | Kisa mafunzo kuhusu mtawanyiko wa watu na matumizi ya rasilimali, video yenye maudhui ya matokeo ya mtawanyiko wa watu katika matumizi ya rasilimali | |
| | | (c) Kumudu matumizi ya mbinu za kuchopeka masuala mtambuka katika ufundishaji na ujifunzaji wa uhusiano kati ya mtawanyiko wa watu na matumizi ya rasilimali | Mbinu za kuchopeka masuala mtambuka katika ufundishaji na ujifunzaji wa uhusiano kati ya mtawanyiko wa watu na matumizi ya rasilimali zimetumika | Video na kisamafunzo chenye maudhui ya masuala mtambuka yanayohusu mtawanyiko wa watu na matumizi ya rasilimali | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (d) Kumudu matumizi ya mbinu za kuchopeka TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa uhusiano kati ya mtawanyiko wa watu na matumizi ya rasilimali | Mbinu za kuchopeka TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa uhusiano kati ya mtawanyiko wa watu na matumizi ya rasilimali zimetumika | Atlasi za kidijitali | |
| | | (e) Kumudu matumizi ya mbinu nyinginezo za ufundishaji na ujifunzaji wa uhusiano kati ya mtawanyiko wa watu na matumizi ya rasilimali | Mbinu nyinginezo za ufundishaji na ujifunzaji wa uhusiano kati ya mtawanyiko wa watu na matumizi ya rasilimali zimetumika | Ramani zinazohusu mtawanyiko wa watu na mtawanyiko wa rasilimali | |
| | 1.6 Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa utunzaji wa mazingira na tabianchi | (a) Kumudu matumizi ya sanaa na michezo katika ufundishaji na ujifunzaji wa utunzaji wa mazingira na tabianchi | Sanaa na michezo katika ufundishaji na ujifunzaji wa utunzaji wa mazingira na tabianchi imetumika | Matini na video mbalimbali zinazohusu namna ya kuratibu shughuli za ufundishaji na ujifunzaji nje ya darasa | 60 |



Muhtasari wa mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa Jiografia na Mazingira, Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi.indd 14 19/10/2024 14:35

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) Kumudu matumizi ya mbinu anuai za ufundishaji na ujifunzaji wa utunzaji wa mazingira na tabianchi katika darasa kubwa | Mbinu anuai za kukabiliana na darasa kubwa katika ufundishaji na ujifunzaji wa utunzaji wa mazingira na tabianchi zimetumika | Video yenye maudhui ya utunzaji wa mazingira na tabianchi | |
| | | (c) Kumudu matumizi ya mbinu za kuchopeka masuala mtambuka katika ufundishaji na ujifunzaji wa utunzaji wa mazingira na tabianchi | Mbinu za kuchopeka masuala mtambuka katika ufundishaji na ujifunzaji wa utunzaji wa mazingira na tabianchi zimetumika | Video na kisamafunzo chenye maudhui ya masuala mtambuka yahusuyo utunzaji wa mazingira na tabianchi | |
| | | (d) Kumudu matumizi ya mbinu za kuchopeka TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa utunzaji wa mazingira na tabianchi | Mbinu za kuchopeka TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa utunzaji wa mazingira na tabianchi zimetumika | Video yenye maudhui ya utunzaji wa mazingira na tabianchi | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (e) Kumudu matumizi ya mbinu nyinginezo za ufundishaji na ujifunzaji wa utunzaji wa mazingira na tabianchi | Mbinu nyinginezo za ufundishaji na ujifunzaji wa utunzaji wa mazingira na tabianchi zimetumika | | |
| | 1.7 Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa Jiografia na Mazingira nje ya darasa | (a) Kumudu matumizi ya mbinu za usimamizi wa shughuli za ufundishaji na ujifunzaji wa Jiografia na Mazingira nje ya darasa | Mbinu za usimamizi wa shughuli za ufundishaji na ujifunzaji Jiografia na Mazingira nje ya darasa zimetumika | Video na matini mbalimbali zinazohusu namna ya kuratibu shughuli za ufundishaji na ujifunzaji nje ya darasa | 40 |



Muhtasari wa mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa Jiografia na Mazingira, Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi.indd 16 19/10/2024 14:35

## Bibliografia


Cambridge International. (h.t). *Creating a Supportive Environment: Great Teaching Toolkit*, https://www.cambridgeinternational.org/support-and-training-for-schools/teaching-cambridge-at-your-school/great-teaching-toolkit/.

The Government of Ireland. (1999). *Primary School Curriculum Geography. Social, Environmental and Scientific Education.*

Levy, C. (1992). *Gender and the environment: the challenge of cross-cutting issues in development policy and planning*. Environment and Urbanization, 4(1), 134-149.

Taasisi ya Elimu Tanzania (2019). *Muhtasari wa mbinu za kufundishia somo la Maarifa ya Jamii kwa mwalimu tarajali, Astashahada ya Elimu Msingi*. Taasisi ya Elimu Tanzania.

Taasisi ya Elimu Tanzania (2019). *Mwongozo wa mwalimu wa kufundisha somo la Maarifa ya Jamii Elimu za Msingi*. Taasisi ya Elimu Tanzania.

Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania (2004). *Sera ya Elimu Tanzania*. Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (2019). *Muhtasari wa Somo la Maarifa ya Jamii Elimu Msingi Darasa la III-VII.* Taasisi ya Elimu Tanzania.